


Mbegu Ndogo: Hadithi ya Wangari Mathai

Wangari Mathai



Nicola Rijdsdijk ✎
Maya Marshak 🎨
Ursula Nafula 📄
Kiswahili 😊
Level 3 📖

(imageless edition)




Storybooks Canada storybookscanada.ca


Mbegu Ndogo: Hadithi ya Wangari
Mathai

Written by: Nicola Rijdsdijk
Illustrated by: Maya Marshak
Translated by: Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.




This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>




Katika kijiji kimoja kwenye mteremko wa Mlima wa Kenya, katika Afrika Mashariki, msichana mdogo alifanya kazi za shambani pamoja na mama yake. Msichana huyu alitwa Wangari.

Wangari alipenda kufanya kazi za nje.
Alitumia jembe kuilima katika bustani ya
familia yake. Kisha alipanda mbegu ndogo
katika ardhi yenye virutubisho.







Alipenda majira ya jioni, wakati jua linapozama. Giza lilipozidi mpaka alishindwa kuona mimea tena, Wangari alifahamu wakati wa kwenda nyumbani uliwadia. Angefuata kijia chembamba kilichopita uwanjani huku akivuka mito akielekea nyumbani.




Wangari alifariki mwaka 2011, lakini tunaweza kumkumbuka kila tunapona mti maridadi.




Wangari alikuwa mtoto mwevu na alikuwa na hamu ya kwenda shule. Lakini wazazi wake walitaka awasaidie nyumbani. Alipofika umri wa miaka saba, kaka yake aliwashawishi wazazi wake kumwacha aende shule.




Wangari alikuwa amefanya bidii. Watu ulimwengu mzima walifahamu hili na wakampa tuzo. Tuzo hili linaitwa, 'Tuzo la Amani ya Nobel.' Na alikuwa mwanamke wa Kiafrika wa kwanza kupokea tuzo hilo.




Alipenda kusoma! Wangari alijifunza zaidi na zaidi na kila kitabu alichokisoma. Alifanya vyema sana shuleni hadi akaalikwa kwenda Marekani kuendeleza masomo yake huko. Wangari alitiwa hamasa sana na nafasi hii! Alipenda kujua ulimwengu zaidi.




Muda ulipopita, miti mipya ilikuwa misitu, na mito ilianza tena kupitisha maji. Ujumbe wa Wangari ulienea Afrika nzima. Leo, mamilioni ya miti imemea kutokana na mbegu za Wangari.




Alipokuwa chuoni huko Marekani, Wangari alijifunza mengi mapya. Alisomea mimea na jinsi inavyokua. Na alikumbuka maisha yake yalivyokuwa utotoni: kucheza michezo na ndugu zake katika kivuli cha miti maridadi ya misitu wa Kenya.



Wangari alijua la kufanya. Aliwafundisha wanawake jinsi ya kupanda miti kutokana na miche. Wanawake waliuza ile miti na pesa walizopata walizitumia kwa mahitaji ya familia zao. Wanawake walifurahi. Wangari alikuwa amewasaidia kuwa wenye nguvu na uwezo.



Jinsi alivyojifunza ndivyo alivyofahamu kuwa aliwapenda watu wa Kenya. Alitaka wafurahi na wawe wenye uhuru. Jinsi alivyojifunza ndivyo alikumbuka kwao nyumbani Afrika.



Alipokamilisha masomo yake, alirudi Kenya. Lakini nchi yake ilikuwa imebadilika. Kulikuwa na mashamba makubwa kila upande. Wanawake hawakupata kuni za kuwasha moto wa kupikia. Watu walikuwa maskini na watoto walikuwa na njaa.